# IMANI NDIO UFUNGUO MAALUM KWA WATOTO WA MUNGU WA KUFUNGUA BARAKA ZAO WANAZOZIHITAJI KUTOKA KWA MUNGU

# MAANDIKO: EBR. 10: 38 - 39, 1YOH. 5: 4 – 5

1. **UTANGULIZI:**

   Kwa vipindi viwili mfululizo nimekuwa nazungumzia juu ya ***Efes. 3: 20 – 21*** (yaani nguvu ya ajabu mno inayowekwa ndani yetu baada ya kuokoka na kisha kujawa na Roho Mtakatifu; nguvu ambayo husababisha tuweze kufanya yale ambayo huko nyuma kabla ya wokovu tulikuwa hatuyawezi.

- Mara ya mwisho nimezungumza juu ya nguvu ya mawazo ya mtu aliyeokoka na nikasema ya kwamba **mwonekano** wa mteule wa nje ni matokeo ya jinsi **anavyowaza** ndani ya moyo wake; **yaani huwezi kutenganisha muonekano wa mtu wa nje na jinsi anavyowaza ndani ya moyo wake**. ***Mith. 23:7 (*****for as he thinks in his heart, so is he**), ni kama ambavyo huwezi kutenga mbegu na mmea (mbegu ndani yake unatokea mmea). Lakini ni lazima mbegu ipandwe kwanza ndipo mmea utokee baadaye.
- **Sasa nguvu hii ya ajabu ikiwa tele ndani ya roho ya mtu wa Mungu; nguvu hii ndiyo itakayomwezesha kufanya maamuzi ya kumtii Mungu na kumwamini kabisa bila kuogopa jambo lolote ambalo litatokea katika maisha yake; na mtu kama huyu ndiye anayeweza sasa KUISHI KWA IMANI BILA KUSITASITA WALA KUOGOPA LOLOTE**

2. **Kuishi kwa imani** ni kuishi maisha ya **asilimia 100** ukiwa na hakika na kazi kamilifu aliyoifanya Yesu Kristo pale msalabani, na bila kutilia shaka ya aina yoyote **NENO** la Mungu lililoandikwa pamoja na **AHADI** zake kwako. ***Kut. 14:10-14***

   **Note: Namna pekee ya kumtambua mteule aliye na nguvu hii ya Mungu ndani ya roho yake inayomwezesha kufanya maamuzi makubwa yanoyoikatalia nafsi yake kufuata**

**matakwa ya mwili wake na kuwa tayari kuishi kwa kumtegemea Mungu pamoja na Neno lake kuwa ndiyo sauti ya mwisho ni tabia zake atakazozionyeshwa wakati wote**

a. **Tabia yake ya kwanza** kabisa ni pale atakapokuwa na tabia ya **kupuuza** kauli za shetani na wakuu wake wakati wote; kauli za vitisho na majigambo ya adui kinyume na Mungu aliye hai. ***Dan. 3:15-23, 1Saml. 17:31-50, 2Wafl. 18:17-37, 2Wafl. 19:1-37*** (mfano Daniel na wenzake, Daudi, Mfalme Hezekia n.k

b. **Tabia ya pili ya mtu aliye na** nguvu za rohoni mwake zinazomwezesha kufanya maamuzi magumu yanayoigomea nafsi yake kufanya matakwa ya mwili ni ule **uwezo wake wa kukiri ukuu wa Mungu wakati wote hata mbele ya adui zake na mbele ya shetani.** ***Kut. 14:10-14, Hes. 14:1-9, Zab. 118:16-17, Ayub. 19:25-27, Isay. 33:13.*** **(**uwezo wa kukiri ukuu wa Mungu wakati unakabiliwa na mazingira magumu hata ya kifo siyo wa mtu wa mwilini tena au mwanadini. ***Mdo. 7:54-60***

c. **Tabia ya tatu** kuu sana ndani ya mteule ambaye nguvu za Roho Mtakatifu imekalia na kutawala kabisa roho yake ni pale ambapo **hayupo tayari kukatishwa tamaa kamwe na watu au mazingira kuhusiana na imani yake**. ***Mdo. 21:9-14, 1Samwl. 17:28-37, Ruth 1:8-18, Math 15:21-28, 1Wafl. 18:41-46, 2Wafl. 2:1-14***. (Nguvu hii ikijaa ndani ya mteule, ni kama chumvi **inapokolea** katika nyama na kisha nyama hiyo inabadilika kabisa sura yake na hofu ya nyama kuoza inapotea kabisa).

d. Anakuwa na tabia ya nne ya kuona vitu (uwezo wa kuona vitu) tofauti na ulimwengu huu unavyoona!!. ***Kut.14:10-14, Luk. 19:41-44, (Luk. 10:21-24), 1Yoh. 5:4-5.*** (wakati wengine wanaona majitu yanayotisha, yeye anawaona kama panzi wa kuliwa tu mbele ya Mungu wake mkuu sana. ***Hes.14:4-9***

**Note: Imani ndani ya mteule ndiyo nguvu iliyo hai kabisa ambayo inamwezesha mteule kukabiliana na milima mbali mbali ya maisha, Imani ndilo jibu halisi kwa matatizo sugu yanayoletwa na adui, Imani**

**ndiyo fimbo; ndilo jiwe analotumia Mungu kumpiga Goliathi, ndiyo nguvu kabambe ya kutuvusha mto Yordani, ndiyo nguvu inayoaangusha kuta walizozitumainia wakuu wa Ulimwengu huu. Imani ndiyo pekee itakayo mtofautisha mteule na Ulimwengu huu**

e. Anakuwa na tabia ya **kuyaishi matamko yake.** ***2Wafal. 5:8-14, Mark. 11:22-24, Math. 8:5-13.*** Kuamini kabisa kwamba jinsi unavyotamka ndivyo itakavyokuwa baadaye ni nguvu ya ajabu sana ndani ya roho ya mtu***. 1 Wafal. 17:1***. Imani ndiyo ufunguo wa kila kitu kwa wana wa Mungu ambao Yesu amewapa. ***Math. 18:18, Yoh. 20:21-23.*** Mfano wangu wa kuzaa watoto wetu

f. Atajaa tabia ya **kupuuza** anasa na tamaa za mwili na kuwa tayari kufanya mambo ambayo yanamtukuza Yesu pamoja na watakatifu wa Mungu. ***Ebr. 11:23-27, Est. 4:16-17, Filip. 3:7-11***

3. **Imani wapendwa ndiyo siri ya ajabu sana iliyowafanya wenzetu waliotutangulia kupata ushindi katika maeneo yote ya maisha yao kiroho na kimwili; ni mamlaka ya ajabu sana kwa mteule kama anataka kuishi kama mtawala wa vitu vyote katika Ulimwengu huu wa sasa**; kumbuka hata Mungu aliumba vitu kwa kutamka na vikatokea. ***Mwanz 1:1-5***

   Tayari Yesu ametumiminia mafuta ya Kifalme juu yetu; na utisho wa Kifalme uko juu yetu, jukumu kubwa lililobakia ni sisi kuishi kwa imani bila hofu wala kusitasita tena ili tumpendeze Yesu wetu.

- Daudi mtu wa Imani anasema "***Zab. 13:1-2***. Hata lini adui yangu atambe na kujitukuza juu yangu lazima ang,oke tu katika Jina la Yesu. Ebu kila mmoja wetu ainuke sasa na akabili milima yote iliyo mbele yake kuwapigania wale wote wanaojitosa kupambana na adui kwa Imani. **Amina.**

***Na***
***Askofu Dr. L. M. Mwizarubi***
***6 March 2022***